Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L.P. 03,
KAKONKO.

Simu Na. +255(028) 2988881
Fax Na. +255(028) 2988881
E-mail.ded@kakonkodc.go.tz
Tovuti : www.kakonkodc.go.tz

***Unapojibu tafadhali taja:***

Kumb.Na.HW/KNK/PF/S.40/5/VOL.IV/68 20.06.2025

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya kakonko anayo furaha kutangaza nafasi 26 za ajira ya Mkataba kwa wananchi wa Kakonko wote wenye sifa stahiki nafasi ya **Wakusanya Mapato.**

- **Sifa za Kuajiriwa.**
  - Awe amehitimu kidato cha nne
  - Awe na umri kuanzia miaka kumi na nane (18) hadi Arobaini na tano (45)
  - Awe na kitambulisho cha Nida au Namba ya Nida
  - Awe anaweza kutumia simu janja.

**1. MASHARTI YA JUMLA**

I. Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania.
II. Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18-45.
III. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
IV. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika na majina mawili ya wadhamini.
V. Maombi yaambatanishwe na picha moja (Passport size ya hivi karibuni na iandikwe jina kwa nyuma).
VI. Waombaji wote waambatanishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ambao hawana vitambulisho hivyo, namba za NIDA ziandikwe kwenye maelezo (CV)
VII. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **27/06/2025** saa tisa alasiri.
VIII. Waombaji wote waambatanishe nakala ya cheti cha kidato cha nne(4)
IX. Maombi yote yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji kwa anuani ifuatayo;

Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 03,

Ndaki S. Mhuli
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**KAKONKO.**